**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OR-TAMISEMI MHE.GEORGE SIMBACHAWENE (Mb.) KWENYE UFUNGUZI WA MKUTANO MKUU WA NNE WA MWAKA WA UMOJA WA MAAFISA ELIMU WA MIKOA NA WILAYA TANZANIA BARA (REDEOA) TAREHE 23/3/2017 KATIKA UKUMBI WA CHUO CHA MIPANGO, DODOMA.**

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Dodoma,

Mhe. Mkuu wa Wilaya Dodoma,

Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais - TAMISEMI

Katibu Mkuu – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,

Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma,

Naibu Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais - TAMISEMI na

Naibu Katibu Mkuu – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Dodoma,

Mwenyekiti wa REDEOA,

Kamishna wa Elimu,

Wakurugenzi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Taasisi zake

Mtendaji Mkuu wa ADEM

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa REDEOA,

Wanahabari,

Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na uzima wa kutuwezesha kukutana tena katika kikao hiki muhimu cha Umoja wa Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya (REDEOA)Tanzania Bara.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika mkutano wa mwaka wa Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya Tanzania Bara (REDEOA).

Aidha, nimefurahishwa sana na kauli mbiu ya Mkutano Mkuu huu ambayo inasema *"**Elimu bora bila malipo inaleta usawa katika jamii**"*. Kauli mbiu hii inaendana na hali halisi ya utendaji wa Serikali ya Awamu ya Tano ya **HAPA KAZI TU!**

**Ndugu, Mwenyekiti,**

Mkutano huu unafanyika katika muda muafaka kwa sababu matokeo ya Mitihani na Upimaji kwa Darasa la Nne, Darasa la Saba, Kidato cha Pili na Kidato cha Nne yamekwishatoka. Hivyo basi, kwa kutumia mkutano huu mnatakiwa kufanya tathmini ya mafanikio na changamoto zinazoikabili sekta ya Elimu hususan Elimu ya Msingi na Sekondari na kuweka mikakati na njia bora za kutatua changamoto hizo. OR -

TAMISEMI iliwaelekeza Makatibu Tawala Mikoa kwakutumia wathibiti Ubora wazikague shule 10 za mwisho katika Mtihani wa Darasa la Saba mwaka 2016. Naamini mtazitumia taarifa hizo katika majadiliano ili kupata majawabu. Lakini pia ni vyema mkabadilishana uzoefu na maafisa elimu ambao shule zao zimefanya vizuri ilikupata uelewa wa pamoja.

Kupitia risala yenu, nimepokea changamoto mbalimbali mnazokumbana nazo ambazo zinaathiri utendaji wenu wa kazi wa siku kwa siku. Baadhi ya Changamoto zilizotajwa nyingi ni za kiutendaji zaidi na mimi nitazitolea maelezo baadhi na nyingine nimekuja na Wataalam wangu mtakaa pamoja mjadiliane kitaalam na mapendekezo yenu watawasilisha kwangu.

Nitaje tu baadhi ya changamoto mlizoziainisha:

1. **Upatikanaji wa Usafiri kwa Maafisaelimu wa Mikoa na Wilaya**.

Suala la usafiri ni muhimu katika kuhakikisha kuwa masuala ya elimu yanatekelezwa vema. Mwaka jana niliagiza Makatibu Tawala wa Mikoa pamoja na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga fedha za ununuzi wa magari kwenye bajeti za Mikoa na Halmashauri. Aidha, nilielekeza kuwa katika kipindi cha mpito Mikoa na Halmashauri zitenge gari zuri na imara kwa ajili ya idara ya Elimu katika ngazi hizo.

Hivyo ni wakati muafaka sasa kufanya ufuatiliaji wa kina kuona mikoa na Halmashauri zilizotekeleza na ambazo hazijatekeleza.

2. **Fedha za matumizi mengine (OC) kutengwa kidogo.**

   Serikali ya Awamu ya Tano imeweka kipaumbele kwa ajili ya fedha za uendeshaji wa shughuli za Serikali na fedha za miradi ya maendeleo. Jitihada zinazoendelea kwa sasa ni kuongeza ukusanyaji wa mapato ili kuinua kiwango cha bajeti ya Serikali kwa kadiri uchumi utakavyo imarika na kuongeza uwezo wa kugharamia uendeshaji wa Serikali. Aidha Serikali imekuwa ikitoa fedha za ufuatiliaji kupitia miradi ya LANES, EQUIP-T, P4R na TUSOME PAMOJA.

   Hivyo, niwasihi sana kuwa mnachokipata kitumieni kwa uaminifu na uadilifu wa hali ya juu.

3. **Upungufu mkubwa wa Walimu katika Shule za Msingi na Sekondari.**

   Ninatambua kuwa bado upo upungufu mkubwa wa walimu kwa shule za msingi na walimu wa Sayansi na Hisabati kwa shule za sekondari. Kigezo cha kupanga walimu wa shule za msingi kwa kutumia uwiano wa walimu na wanafunzi (PTR) kinazinyima shule zenye wanafunzi wachache haki ya kupata walimu wa kutosha na hivyo kukosa ufanisi wa kuweza kufundisha kuanzia darasa la

Awali hadi VII. Aidha, shule na vitengo vya wanafunzi wenye mahitaji maalum huathirika zaidi, kwa walimu kuonekana hawana kazi za kutosha kwa kuwa wana idadi ndogo ya wanafunzi. Kwa sasa OR-TAMISEMI inatumia mikondo katika kupanga walimu wa shule za msingi kwa lengo lakuleta uwiano sawa hasa kwa shule zenye wanafunzi wachache.

Kwa upande mwingine Serikali imeanza kupunguza walimu wa ziada wa masomo ya Sanaa wa shule za Sekondari na kuwapanga katika shule za Msingi. Tayari zoezi hili limeanza katika Mkoa wa Arusha ambapo zaidi ya walimu **700** wa ziada wa masomo ya sanaa wamehamishiwa shule za msingi.

Kwa upande wa shule za Sekondari Serikali itaendelea kuajiri walimu wa Sayansi na Hisabati hadi shule zote zipate walimu wa masomo hayo wa kutosha. Kwa sasa tunaendelea kuwapangia vituo walimu wapya **3102** wa Sayansi na Hisabati. Kuna upungufu wa walimu **1027** kwenye kibali cha walimu wapya **5129** wa Hisabati na Sayansi kilichotolewa mwezi Februari 2016. Naomba walimu wote waliomaliza ualimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati kabla ya mwaka 2015 wajitokeze kuomba.

**4. Upungufu wa Miundombinu na Maabara.**

Wizara yangu inatambua upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, Matundu ya vyoo kwa upande wa shule za Msingi na shule Sekondari na maabara kwa upande wa Sekondari. Hadi sasa Serikali imejenga maabara **290** kupitia SEDP II

na kukarabati maabara **255** kwa fedha za P4R. Kwa upande mwingine Serikali imenunua vifaa vya maabara kwa shule **1696** za Serikali.

5. **Kuchelewa kwa fedha za mitihani**

Wizara yangu inatambua changamoto zilizojitokeza katika zoezi zima la uendeshaji wa mitihani ikiwemo madeni ya wasimamizi na wazabuni.

Serikali itaweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha fedha hizo zinafika kwa wakati kwenye Mikoa na Halmashauri. Aidha, madeni yanayohusiana na uendeshaji wa Mtihani wa Kidato cha Nne, 2015 na kidato cha Pili na Darasa la Nne mwaka 2016 yamewasilishwa HAZINA ili taratibu za malipo ziweze kufanyika.

6. **Kuongeza kiwango cha fedha za ruzuku ya uendeshaji, fidia ya ada pamoja na fedha za chakula cha wanafunzi**.

Tunatambua kuwa gharama za uendeshaji wa shule zimepanda na jambo hili Serikali inalielewa. Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wanakamilisha utafiti wa kubaini gharama halisi ya kumsomesha mwanafunzi kwa mwaka kwa kuzingatia mazingira ya shule ilipo (unit cost). Majibu ya utafiti huu yataisaidia ofisi yangu kujua gharama halisi ya uendeshaji wa shule zetu.

7. **Wanafunzi wenye mahitaji maalum kutotengewa fedha zaidi katika ruzuku ya uendeshaji**.

Utaratibu uliopo sasa, Wanafunzi wenye mahitaji maalum hutengewa fedha sawa na wanafunzi wa kawaida. Ushauri mlioutoa ni wa msingi, hivyo, utafanyiwa kazi. Hata hivyo, Serikali imeendelea na utaratibu wa kununua vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum ili kuzipunguzia changamoto shule hizo. Hadi sasa vifaa vya zaidi ya Sh. Billioni **4.2** vimenunuliwa na usambazaji wa vifaa utaanza muda si mrefu kwa shule na vitengo vyote nchini.

8. **Wanafunzi wa Elimu ya Awali kutotengewa rasilimali fedha/ watu**.

Kwa sasa changamoto hii imeshughulikiwa. Katika takwimu zilizowasilishwa HAZINA kuomba fedha, Darasa la Awali limejumuishwa. Kwa upande mwingine Serikali imetoa mafunzo kwa walimu wa elimu ya awali **16,129** kwa shule zote za msingi nchini. Lakini pia, walimu wahitimu wa ngazi ya cheti mwaka 2015, wanaotarajia kuajiriwa hapo baadae, wanao ujuzi na maarifa ya kufundisha Elimu ya Awali. Naomba nisisitize kwamba wanafunzi wa Elimu ya Awali ni sehemu kamili ya shule za msingi, hivyo wajumuishwe katika bajeti na mipango yote ya shule husika**.**

## 9. Kuboresha Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule

Serikali kwa sasa ipo kwenye utaratibu wa kuboresha Idara ya Uthibiti Ubora wa shule ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Katika kuimarisha idara hii, jumla ya magari **41** yamenunuliwa na kukabidhiwa kwa wathibiti ubora wa shule ngazi ya Wilaya. Aidha, katika mpango wa P4R idara hii imepewa uzito unaostahili, sambamba na kwenye mpango wa LANES ambapo imetengewa sehemu ya fedha kwa ajili ya ukaguzi.

## 10.Ruzuku ya Uendeshaji ya dola 10 na dola 25 za sasa.

Mwaka 2002 Serikali ilianza kutoa ruzuku ya uendeshaji kwa shule za Msingi na Sekondari kwa kiwango cha **shilingi 10,000/=** kwa shule za Msingi na **shilingi 25,000/=** kwa shule za Sekondari. Fedha hizo zilikuwa ni msaada kutoka kwa wahisani kwa makubaliano ya muda maalum. Muda huo umekwisha na sasa Serikali inagharamia kwa kupitia mapato yake ya ndani. Toka wakati huo kiwango hicho hakijabadilika kwa kuwa makusanyo ya Serikali bado hayajakidhi gharama halisi za uendeshaji kutokana na kupanda kwa gharama za uendeshaji. Nia ya Serikali ni kuongeza kiwango hicho mara kwa mara pindi hali ya makusanyo itakapokuwa ya kuridhisha.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Baada ya kutoa ufafanuzi kuhusiana na changamoto zilizoelezwa katika risala yenu napenda nichukue fursa hii kutoa maagizo na maelekezo ya uendeshaji wa elimu.

**Ndugu Mwenyekiti,**

**Falsafa ya ElimuMsingi bila Malipo.**

Serikali, kupitia Waraka wa Elimu Na.5 wa mwaka 2015 imeamua kutoa Elimumsingi (kuanzia Elimu ya Awali hadi Kidato cha Nne) bila malipo. Azma hii ya Serikali ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015-2020 na maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli aliyoyatoa wakati akizindua Bunge la Kumi na moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Elimumsingi bila malipo ina maana kwamba mwanafunzi atasoma bila mzazi/mlezi kulipa ada wala michango ya lazima ya fedha iliyokuwa ikitozwa shuleni kabla ya kutolewa kwa Waraka **wa Elimu Namba 5 wa mwaka 2015.**

Mwanafunzi yeyote asiyehudhuria siku 5 hatua zichukuliwe dhidi ya mzazi/mlezi, na badala ya kusubiri siku 90 ili afukuzwe.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Katika kutekeleza Elimumsingi bila malipo kuna majukumu ya Serikali, wazazi/walezi,wakuu wa shule na Kamati/Bodi za shule na jamii kwa ujumla, kama ilivyoelezwa kwenye Waraka wa Elimu Na 5 wa Mwaka 2015 na Miongozo mbalimbali iliyotolewa. Hivyo ninatoa wito kwa kila mmoja wenu kutimiza wajibu katika eneo lake.

Serikali kwa upande wake inafanya juhudi kubwa kugharamia Elimumsingi, Kwa sasa kiasi cha **Shilingi Bilioni 20.8** kinatolewa kila mwezi kwa shule za Msingi na Sekondari ikiwa ni fedha ya kugharamia elimu bila malipo zikiwemo **Sh. Bilioni 5.1** posho za Madaraka kwa Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Waratibu Elimu Kata. Kwa upande mwingine Serikali inakamilisha kusambaza vitabu vyote vya **darasa la I – III** na **kidato cha 1-6.** Kadhalika vifaa na kemikali za maabara kwa shule za Sekondari nchini vimenunuliwa.

**Ndugu Mwenyekiti,**

**Uandikishaji wa Wanafunzi wa Darasa la Kwanza, Awali na Kidato cha Kwanza 2017**

Tumepata mafanikio makubwa katika uandikishaji wa wanafunzi wa Elimu ya Awali na wale wa darasa la kwanza. Hadi tarehe 15/3/2017 jumla ya wanafunzi **1,251,002** wa awali, **1,720,003** wa darasa la kwanza na **476,610** wa kidato cha kwanzawalikuwa wameandikishwa. Aidha, hakikisheni hakuna uandikishaji mpya baada ya tarehe 31/3/2017.

Tarehe hii ndio mwisho wa uandikishaji na ndio siku ya sensa ya wanafunzi wa shule za Msingi na Sekondari hapa nchini.

Mafanikio hayo ya uandikishaji yameibua changamoto za upungufu wa miundombinu ya kutosha vikiwemo vyumba vya madarasa, madawati na kwa baadhi ya shule hasa za vijijini kuwa na mahitaji zaidi ya walimu. Ilikukabiliana na Upungufu huo, tayari Serikali imetoa kiasi cha **Shilingi Bilioni 22** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika shule za Sekondari **85** na za Msingi **19** nchini ujenzi unatakiwa kukamilika ifikapo Juni 2017.

Aidha, Halmashauri zote zimeagizwa kuhakikisha kuwa vyumba vya madarasa vinajengwa kwa kuzingatia idadi ya wanafunzi waliopo kwa sasa. Kupanga ni Kuchagua!

**Ndugu Mwenyekiti,**

Nimesikitishwa sana na zoezi la uhakiki wa madeni ya walimu madeni yaliyowasilishwa mwezi Aprili 2016, yalikuwa ni **Shilingi Bilioni 26**, kati ya hayo deni lililokubaliwa ni la takriban **Shilingi bilioni 9.8** tu. Hii inamaanisha kuwa madeni yaliyowasilishwa hayakuwa sahihi. Tafsiri yake ni kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa hazikuwa makini katika uhakiki huo. Ninatoa rai kwenu kwamba kuanzia sasa, yeyote atakayewasilisha deni au taarifa isiyo sahihi atawajibishwa bila huruma.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Msingi wa Sera ya Elimu na Mafunzo na utoaji wa Elimu kwa Taifa letu unajikita katika kumjengea Mtanzania msingi bora wa malezi, maadili, ujuzi, umahiri na kumwezesha kujitegemea.

Mpango wa Elimu ya kujitegemea utawafanya wanafunzi wafanane na maisha ya kitanzania na kuwafanya watambue wajibu wao kwa jamii kufuatana na ujuzi walioupata baada ya kumaliza shule na vyuo. Aidha, Elimu ya kujitegemea itasaidia upatikanaji wa chakula shuleni kwa ajili ya wanafunzi. Kwa muda mrefu sasa Elimu ya kujitegemea imeachwa kabisa katika shule zote za Msingi na Sekondari.

Ninatoa wito kwenu, kuhakikisha elimu ya kujitegemea inatekelezwa kikamilifu, kwa kuhakikisha kila shule ina shughuli mbalimbali za uzalishaji mali kama vile mashamba ya chakula na bustani za mbogamboga katika maeneo ya shule.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Kabla sijamaliza hotuba yangu ningependa niseme juu ya Mapungufu ambayo yamekuwa yana athiri Ubora wa Elimu hapa nchini.

**(i) Tatizo la Upatikanaji wa Takwimu sahihi**

Nimekua napata wakati mgumu kila mara ninapohitaji takwimu mbali mbali kutoka Idara ya Elimu ya OR-TAMISEMI. Ukiuliza leo idadi ya Shule zote nchini utaambiwa idadi fulani, kesho yake ukiuliza unapata idadi tofauti kabisa na idadi ya jana! Takwimu za maeneo mengi ni za kupika na Wapishi wa Takwimu hizo ni nyie Maafisa Elimu kutoka RS na LGAs mnawapa *wrong data/cooked data*! Hamuendi kwenye *field* mnakaa maofisini muda wote.

Lakini pia ipo haja ya kujiuliza hivi Maafisa Elimu Vifaa na Takwimu ni Watu waliosomea Takwimu? Au tunawapa vyeo kisa wamesomea Ualimu?

Mimi nadhani ipo haja sasa tuamue kuteua Wataalamu waliosomea masuala ya Takwimu ambao pia wanauwezo wa kuzielezea takwimu hizo kwa mapana zaidi. Inashangaza unakuta Afisa Elimu Takwimu hajui hata kutumia komputa!

**(ii) Visingizio na Kutowajibika Ipasavyo:**

Shughuli nyingi zinazofanyika kwenye LGAs na RS hazina usimamizi thabiti **"Hakuna Ownership"** Visingizo na kutojali kuna anzia kutoka kwa Afisa Elimu Mkoa hadi Mwalimu Mkuu wa Shule husika, umekosekana uelewa wa kutambua kuwa wao ndio wasimamizi wa shughuli mbalimbali zinazoendelea katika maeneo yao husika. Wakati mwingine Viongozi tunapewa taarifa za uongo kwenye ziara, una ambiwa Jengo limefikia Asilimia 80, lakini ukisema twende tukaone unakuta kifusi cha mchanga tu au msingi! Na wakati mwingine akianza kukupeleka anapotea njia, hapakumbuki vizuri! Nimeshuhudia hili kwenye Ukaguzi wa Miradi ya SEDP II. Bado upo uongo mwingi na Usanii uliokithiri!

**(iii) Matumizi mabaya ya Vyeo:**

Upo unyanyasaji mkubwa unafanywa na baadhi ya Maafisa Elimu, mnapokuwa kwenye maeneo yenu manjifanya ni miungu watu, mnanyanyasa walimu wenzenu mnawatolea lugha chafu, kukomoana, hamuwasikilizi Walimu wenzenu, rushwa za ngono kwa walimu wa kike! Roho mbaya na lugha za vitisho, utanitambua mimi ni nani!

**(iv) Lipo tatizo la kutokidhi uwezo na ufanisi wa nafasi zenu:**

Kuna haja kubwa kuangalia mfumo mzima wa namna ya upatikanaji wa vyeo vyenu, baadhi yenu mmepata nafasi hizi kwa *deal* na kutokana na

hilo imefikia level ya kutomudu majukumu ya nafasi zenu! yaani mtu yupo kwenye nafasi ambayo hakustahili, hawezi kazi! *You have been raised to the level of Incompitence!* Katibu Mkuu nakuagiza ifanyike audit kwa wale ambao hawawezi kumudu majukumu yao tuwapeleke sehemu wanazo stahili, tuachane nao. Hili tutalifanya kwa faida ya kuinua ubora wa Elimu ya Taifa letu.

**(v) Maafisa Elimu kusubiri Ripoti Maofisini:**

Kama nilivyosema awali miingoni mwenu mnakaa sana maofisini na hivyo mnashindwa kupata taarifa sahihi ya nini kinachoendelea kwenye shule zenu, mnasubiri kuletewa taarifa ambazo nazo mnakua mmedanganywa. Mwaka jana nikiwa kwenye ziara Jimboni kwangu nilitembelea shule moja ya Lufu nikaamua kuingia darasa la 4,6 na 7 kuangalia madaftari yao, nilichoshuhudia huwezi amini watoto wanamiandiko mibaya sana haieleweki, lakini mbaya zaidi wengi wao hawajui kusoma na kuandika! Mwanfunzi wa darasa la Saba anasoma kama mwanafunzi wa darasa la Pili. Lakini pia nikagundua tatizo jingine wanafunzi wale wanasahihishana madaftari yao. Yaani kila mwanafunzi ana peni nyekundu. Habari nilizo nazo tatizo hilo lipo nchi nzima wanafunzi wanasahihishana madaftari yao.

**(vi) Ukosefu wa Kipaumbele kwenye Bajeti ya Elimu**

Halmashauri zetu zimekua zikipanga bajeti kwa mazoea, hakuna mikakati ya kumaliza changamoto kwenye sekta ya Elimu. Unakuta Halmashauri ina upungufu wa madarasa 700 na nyumba za walimu 400 lakini kwa mwaka Halmashauri inatenga bajeti ya kujenga madarasa 20 na nyumba za Walimu 30. Kwa utaratibu kama huu hatuwezi kumaliza matatizo hayo kwa Wakati. Naagiza Halmashauri ziandae bajeti zenye uhalisia kutokana na changamoto zilizopo.

**(vii) Uhakiki wa Watumishi hewa**

Lipo tatizo kubwa ambalo limegundulika kuwa Walimu wengi wameondolewa kazini kwa sababu ambazo ni uzembe wa utunzaji kumbukumbu, kundi kubwa la Walimu hao walikua masomoni, Wameonekana ni Walimu hewa kwamba walienda kusoma bila ruhusa. Lakini wengine wana barua kabisa za ruhusa ila barua na kumbukumbu zake hazionekani kwa waajiri wao. Uzembe huu umesababishwa na Maafisa Utumishi kutokuwa makini katika kuweka kumbukumbu sawa. Kutokana na tatizo hili nimeamua kuanzisha Dawati Maalum la kusikiliza malalamiko yote ya aina hiyo kwa Walimu, tangu nitangaze azima hiyo kwenye vyombo vya

habari tarehe 10 Machi 2017 hadi leo tarehe 23 Machi 2017 jumla ya **Malalamiko 105 yamesha wasilishwa** Wizarani.

Niwaombe maafisa Elimu katika ngazi zote kuweni mabalozi wa kusaidia kutatua shida za Walimu wetu, maana wanateseka sana, wanapokuja Halmashauri hawasikilizwi na Maafisa Utumishi na wakija kwenu na nyie mnakua wakali hamuwasikilizi, mnawavunja moyo sana na wengi wa walimu wetu wanakua na msongo wa mawazo.

**Ndugu Mwenyekiti**

Nawasihi sana kupitia umoja wenu wa REDEOA utumieni kuonyana, kufundishana na kupata taarifa za kina za utendaji kazi wenu ili tuweze Kuinua Elimu ya Taifa letu. **Mimi naendelea kuamini hatma ya Elimu ya Nchi yetu ipo mikonni mwenu.**

Mwisho napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru tena, pia naomba wote kwa pamoja tushirikiane ili lengo la Serikali la kutoa Elimumsingi bila malipo liweze kufanikiwa kwani limeleta mafanikio makubwa katika Sekta ya Elimu.

Baada ya kusema hayo natamka kwamba Mkutano huu wa Nne wenye kauli mbiu ***"Elimu bora bila malipo inaleta usawa katika jamii"***

Mkutano huu nimeufungua rasmi.

***ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA.***